

MAMLAKA YA UTHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

TAARIFA KWA UMMA

KUONGEZEKA KWA BEI ZA MAFUTA

1. Mamlaka ya Uthibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) haikuridhishwa na ongezeko la sasa la bei ya mafuta kwa zaidi ya kiwango kilichotarajiwa kutokana na ongezeko la kodi kama ilivyotangazwa katika bajeti ya Serikali ya mwaka 2007/08. Makampuni ya mafuta yameongeza bei kwa kuhusisha ongezeko hilo na kupanda kwa viwango vya kodi na gharama za usafirishaji.
2. Uchambuzi wa kina uliofanywa kwa pamoja na EWURA, Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati na Madini, Mamlaka ya Uthibiti wa Huduma za Usafiri Majini na Nchi Kavu (SUMATRA), na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) umebaini kwamba:-
 - a) akiba ya mafuta iliyokuwepo hadi tarehe 30 Juni 2007 ingetosheleza mahitaji ya Taifa kwa siku zisizopungua 15 kuanzia tarehe 1 Julai 2007;
 - b) tathmini ya kodi husika kwa akiba ya mafuta hayo ilishafanywa na TRA;
3. Kuingiza viwango vya kodi mpya kwenye mfumo wa bei kwenye akiba ya mafuta iliyokwishatathminiwa na TRA ni **MAKOSA**. Kuna ushahidi kwamba mafuta yanayouzwa hivi sasa ni yale ambayo kodi husika ilikwishatathminiwa kabla ya tarehe 1 Julai 2007 kwa kutumia viwango vya zamani vya kodi.
4. Wafanyabiashara wa mafuta wanaotumia kisingizio cha mabadiliko katika viwango vya kodi na kupandisha bei kwenye akiba ya mafuta iliyokwishafanyiwa tathmini na TRA, wanaagizwa kupunguza bei zao mara moja.
5. Aidha kwa kuzingatia ongezeko la kodi la Shs 124 kwa lita kwa mafuta ya petroli (supa), na Shs 122 kwa lita kwa dizeli bei hazikutarajiwa kuzidi Shs 1,400 kwa lita kwa petroli na Shs. 1,365 kwa lita kwa dizeli kwa mafuta yaliyoingizwa nchini **BAADA** ya ongezeko la kodi.
6. Makampuni ya mafuta hayakatazwi kurekebisha bei zao ili ziandane na gharama za uagizaji mafuta pamoja na mabadiliko ya kodi. Hata hivyo katika ongezeko la kodi la hivi karibuni hapakuwa na sababu za msingi za kuongeza bei za mafuta, na hivyo kuilazimu EWURA kutoa maelekezo haya.
7. EWURA inasisitiza kwamba wafanyabiashara ya mafuta hususani makampuni yanayoingiza mafuta nchini, yahakikishe panakuwepo na ushindani halali kwenye

sekta hii, ili kumfanya mlaji afaidike na hali ya ushindani iliyopo katika soko kwa kupata mafuta yenye ubora na kwa bei nafuu.

8. EWURA ina jukumu la kulinda maslahi ya walaji na itaendelea na udhibiti wa sekta ya petroli ili kuzuia tabia ambazo haziendani na sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji wa biashara ya mafuta.

IMETOLEWA NA: MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI
NA MAJI